

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3  
Fax Na: 2152820  
(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe  
kwa Kamishna wa Mamlaka )



8 Barabara ya Kivukoni,  
S.L.P. 80327,  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**UMOJA WA MATAIFA WAIPONGEZA TANZANIA KWA JITHADA ZA UDHIBITI NA  
MAPAMBANO DHIDI YA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA**

**Dar es Salaam, 12 Machi 2020:**

Shirika la Umoja Wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) kupitia Kamisheni ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (CND), limeipongeza Tanzania kwa jitihada madhubuti katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya ambazo zimeleta matokeo chanya katika mapambano ya dawa za kulevya duniani katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2018 hadi 2020.

Katika mkutano wa 63 wa Kamisheni ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya duniani (CND 63) uliofanyika Vienna - Austria, mkuu wa Shirika la Umoja Wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) Bi. Ghada Fathi Wally amesema “Tanzania ni moja kati ya nchi chache barani Afrika, zilizofanikiwa kupunguza upatikanaji na uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kuweza kutekeleza mikakati minne ya kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa uwiano ulio sawa”.

Mafanikio haya yamekuja kutokana juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya marekebisho makubwa ya kisheria kwa kutunga Sheria ya Kudhibiti na

Kupambana na Dawa za Kulevya Sheria Na.5 ya mwaka 2015 na mabadiliko yake ya mwaka 2017 kwa Tanzania Bara, na kwa upande wa Tanzania visiwani ambako mabadiliko ya sheria yamefanyika mwaka 2019.

Pamoja na kuwa na ukanda mrefu wa bahari na ukubwa wa mipaka, Tanzania imeimarisha udhibiti wa mipaka yake kwa kushirikiana vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa kufanya opereheni za mara kwa mara mipakani na majini ambazo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya nchini.

Kutokana na mafanikio hayo, mwaka 2018 Shirika la Umoja Wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) liliipa Tanzania heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa kwa Kanda ya Afrika wa wakuu wa vyombo vinavyopambana na tatizo la dawa za kulevya (HONLEA 28) uliofanyika ukumbi wa mikutano wa Mwl. Nyerere jijini Dar es Salaam.

Aidha, taarifa ya UNODC ya mwaka 2019 inafafanua bayana kwamba Tanzania imefanikiwa kupunguza asilimia 90 ya uingizaji wa dawa za kulevya hususani Heroin zilizokuwa zinaingia kupitia ukanda wa bahari. Shirika hilo la Umoja wa Mataifa pamoja na vitengo vyake lina utaratibu wa kutoa taarifa za kila mwaka juu ya mwenendo wa tatizo la dawa za kulevya duniani.

Pamoja na mafanikio haya makubwa, kwa masikitiko makubwa baadhi ya magazeti wanaichafua nchi yetu kwa kuandika habari zisizosahihi kuhusu udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kimataifa nchi yetu imekuwa ni nchi ya mfano wa kuigwa, kwani hata nchi za Uganda, Msumbiji, Ghana, Nigeria na Norway zimeomba kujifunza kutoka kwetu mfumo wa utendaji kazi wetu pamoja na sheria yetu inavyofanya kazi.

Gazeti la The East African toleo namba 1323 la tarehe 07 – 13 Machi 2020, na gazeti la kimtandao la The Citizen tarehe 8 mwezi Machi 2020 yameandika taarifa inayofanana ikisema Tanzania ni **kitovu** cha dawa za kulevya Afrika Mashariki. Taarifa hizo ni za upotoshaji na zinatakiwa kupuuzwa, kwani nchi yetu ni moja ya nchi zinazofanya vizuri katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya duniani.

Ni muhimu kuwa makini katika uandishi wa habari na ni vema kutumia vyanzo vya uhakika na kuzingatia maadili ya uandishi. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mujibu wa sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kifungu cha 7(2) ina wajibu wa kutoa taarifa sahihi kwa jamii ya watanzania kuhusiana na masuala ya dawa za kulevya, na vilevile vyombo vya habari kwa kifungu hiki vinawajibika kutoa habari sahihi kwa wananchi kinyume na hapo ni ukiukwaji wa Sheria.

Mamlaka iko wazi na tayari wakati wote kutoa ushirikiano hususan kutoa taarifa za masuala mbalimbali yanayohusu dawa za kulevya. Pia, baadhi ya taarifa sahihi zinapatikana kupitia tovuti ya Mamlaka [www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz) na taarifa za dawa za kulevya kimataifa kupitia tovuti ya Shirika la Umoja Wa Mataifa Linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) ambayo ni [www.unodc.org](http://www.unodc.org).

**Imetolewa na,**



Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**